Lead & Earn


# ONGOZA & PATA KIPATO KWA UBUNIFU WAKO

woc@womenonchange.org

1+202-656-0077

Ofisi ya Kimataifa & Kwa Njia ya Mtandaoni

https://www.womenonchange.org


Uongozi
katika Familia
Uongozi
katika Jamii
Uongozi
Wote
Vijana Waleta
Mabadiliko
Duniani

## ONGOZA & PATA KIPATO KWA UBUNIFU WAKO



~~~Maneno machache~~~

**LEXIMA, Jeanose |** Women on Change (WoC) – Mkurugenzi Mkuu

Takribani miaka ishirini iliyopita, nilijiuliza, kama kuna njia ya kuboresha hali ya maisha ya kila mtoto anayekabiliwa na shida kokote alipo duniani kwa kutumia rasilimali kidogo kabisa? Ili kupata jawabu ilinibidi kuingia barabarani kufahamu zaidi juu ya watu wenye watoto, watoto, jamii zilizopo zilizoundwa au kutengenezwa.

Natoa shukrani nyingi kwa wote walionikaribisha nyumbani kwao, katika jamii zao, na kusimulia hadithi zao, watu wengi waliojitolea muda wao. Kwa sauti za pamoja, ninaweza kusema kwa fahari kwamba mwishoni ilibidi nijirudie mwenyewe. Nilitakiwa kujielewa, kuelewa familia, jamii na watu, ambao walikuwa ni sehemu ya maisha yangu, imani za vizazi, maisha, baada ya kutafakari kwa kina, majibu ambayo nilikuwa nikiyatafuta siku zote yalikuwa ndani yangu.

Maisha yangu yamebadilika na siku zote ninajua kwamba kuna mengi zaidi ya yale tunayoyasikia, kusoma na yanayotolewa na kila mtu. Ni muhimu kwangu kuchukua wajibu, kuamini katika hatua zangu katika kutimiza kile nilichotaka kukijua, kadri ninavyoendelea kukua, wakati mwingine inamaanisha ninahisi fahari, lakini kuwa makini na malengo makubwa na kujiamini katika safari yako ya kutafuta kile unachokitafuta.Ni vigumu, kama hauna jamii ya kukuwezesha kupita mchakato huo au unaogopa kuwajibika na kuonekana mjinga. Habari nzuri ni kwamba jamii imekuzunguka, utakapogundua ya kwamba wote sisi ni sehemu ya jamii hii ambayo inatupa maisha yetu, na wakati mwingine, unatakiwa kurudi nyuma kidogo ili uweze kufahamu kile kilichopo ndani yako, kabla ya kukubaliana na maisha ambayo ungependa kuyaishi.

Women on Change ni jamii yako. Tunajenga jamii zinazostawi ulimwenguni kote ili kusaidia watoto kushikilia amani waliyonayo ndani yao. Muda wako, sauti yako, fedha, ujuzi, uzoefu na zaidi vyote vinatusaidia kufanya hivyo.

Tunahitaji ujiunge nasi katika kuandaa urithi wa huduma kwa ajili ya kila mtu kuweza kufikia uwezo wao binafsi wa juu. Ni matumaini yangu programu ya Ongoza na Pata Kipato au Lead & Earn itasaidia jamii yako.

Nashukuru sana kwa kusoma maendeleo yetu!

*Jeanose Lexima*
~~~

## Yaliyomo

1. Programu ya Ongoza & Pata Kipato au Lead & Earn (L&E) ........ 8
I. Uwekezaji ........ 9
II. Uchaguzi wa mawazo ........ 9
III. Chagua majaji kwa ajili ya mawazo ........ 9
IV. Faida kwa Majaji ........ 10
V. Maandalizi kidunia & Ratiba ........ 10
VI. Maeneo ya Matukio ya Kidunia ........ 10
VII. Eneo la kazi ........ 10
2. Maswali ya mara kwa mara (FAQs) na Vidokezo ........ 11
I. Ninajiungaje au kuwa mshirika katika programu hii? ........ 11
II. Tunatoa nini kwa washirika? ........ 11
III. Mahitaji ya kuwa mshirika ........ 11
IV. Tunatafuta washirika wa aina gani? ........ 11
V. Tunawawezeshaje washirika? ........ 11
VIII. Je, tunatoza pesa kufundisha washirika? ........ 12
IX. Uanachama & mafunzo ya WoC ........ 13
X. Malipo ya mtandaoni ........ 13
XI. Ratiba ya Mafunzo ........ 13
VI. Ili kutekeleza programu hii, nifanye nini? ........ 13
VII. Amua muundo wa timu yako ........ 13
VIII. Miongozo ya kufanya kazi kama timu ........ 14
IX. Tambua muundo wako wa ndani wa ufundishaji ........ 15
X. Tazama Waalimu ........ 15
XI. Kuanza ........ 16
XII. Vidokezo vya Kujiandaa-Kabla ........ 16
XIII. Mradi & wazo ........ 17
XIV. Wazo gani au biashara gani ni kubwa? ........ 17
XV. Kwanini kufikiria kunasaidia? ........ 17
XVI. Ushirikiano ........ 18
XVII. Mawazo yaliyochaguliwa ........ 18
XVIII. Kiasi cha uwekezaji ........ 18
XIX. Mipango na kujua ujuzi ........ 18
XX. Changanua&Hakikisha wazo ........ 18
XXI. Kutangaza & Kuuza wazo ........ 19
XXII. Ninajipangaje kwa ajili ya programu yangu (ratiba ba Bajeti)? ........ 19
XXIII. Nitekeleze vipi programu hii? ........ 19

XXIV. Ujasiriamali ni Nini, Ushauri, Kufundisha ..... 20
XXV. Ni Mafunzo, Uponyaji na Tiba gani zinatolewa? ..... 20
XXVI. Mafunzo yapi ya Biashara yanatolewa? ..... 20
XXVII. Utayari wa Chuo & Elimu ..... 20
XXVIII. Tunachukuaje waalimu katika programu yetu? ..... 20
XXIX. Je, tunawalipa waalimu? ..... 21
XXX. Ni mafunzo gani & vitu gani vinavyotolewa ..... 21
XXXI. Jinsi ya kuwasaidia watoto kuwasilisha mawazo yao na kushinda zawadi? ..... 21
XXXII. Jinsi ya kuandaa vijana na mikutano ya kimataifa ..... 21
XXXIII. Uhamasishaji wa Usalama Mtandaoni ..... 22

# ONGOZA & PATA KIPATO KWA UBUNIFU WAKO

**Kuhusu Nyaraka Hii –**Progamu yetu ya Ongoza na Pata Kipato au Lead and Earn imetengenezwa kwa ajili ya kuwezesha jamii, wazazi na vijana kutengeneza maisha yao ya baadae kwa kutumia ubunifu wao. Nyaraka hii inatumika kama mrejesho, pamoja na mafunzo yetu kwa ajili ya kijana yoyote duniani.

**Jambo ambalo hii nyaraka sio –** Nyaraka hii sio ramani ya jinsi ya kuwa mjasiriamali, kuelimisha, kufundisha vijana au kutoa ushauri wa kitaalamu au kwa mawazo mengine.

**Angalizo–**Hatutangazi taarifa za mtandaoni, sera, dini, rangi fulani, uraia, jinsia, takwimu au biashara yoyote iliyotumika katika nyaraka hii.


**Tafsiri**– Nyaraka hii inapatikana bure kwa mtu yeyote aliye na umri wa miaka 18 na zaidi. Ukitafsiri nyaraka hii katika lugha yako, tafadhali tutumie nakala yake. Kupata nakala ya Microsoft Word, tutumie barua pepe kwa woc@womenonchange.org

**Toleo Jipya** –Sehemu ya programu katika nyaraka hii itakuwa mubashara mtandaoni kwa ajili ya kila mtu kuifungua. Wakati huo huo, pokea toleo jipya la PDF na kisha fuata WoCkwenyeyoutube, facebookna twitter.

**Maamuzi**– Tafadhali fanya maamuzi yako yaliyo bora juu ya taarifa zinazopatikana mtandaoni.

**Maswali kuhusu programu –** Tembeleawww.facebook.com/womenonchange maswali&majibu mubashara kila mwezi (Alhamisi ya mwisho)**.**

**Tunaomba mchango wako** https://womenonchange.org/donate-give/



# ONGOZA & PATA KIPATO KWA UBUNIFU WAKO

**1. Programu ya Ongoza & Pata Kipato au Lead & Earn (L&E)**

Programu hii ni mkusanyiko wa masomo tuliyojifunza katika kutekeleza programu za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM) Mentoring Hope, Math Speak, na programu zingine za majaribio ili kuwasiliana vizuri, na kufahamu namna bora ya kushirikiana na jamii zenye uhitaji mkubwa wa rasilimali.

Programu hii ipo maalumu kwa ajili ya kusaidia jamii, wazazi kuwa na ufahamu, kuepusha mishtuko (trauma), kuboresha hali za kiuchumi na kijamii, kwa kusema, kushirikishana ujuzi, kuwekeza muda na fedha katika ubunifu wa vijana mapema.

**Mbinu Yetu** – Tunawekeza, kufundisha, kuwapa ari na motisha wajasiriamali, waalimu wenye ujuzi na watu wanaojitolea wenye miaka 18-30, huku wao wakiwekeza kwa vijana wadogo wenye umri wa miaka 8-18.

- Tunahudumia watu wa miaka 18-40, ambao wako tayari kujitengenezea fursa tembelea hapaili kupata taarifa zaidi.

**Malengo ya Programu**

- Kuongeza ufahamu wa kujielewa ili kujenga kile kinachokusukuma binafsi
- Kukuza uwezo wa kutatua matatizo mapema ili kuja kuongoza
- Kuboresha uelewa wa sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati
- Kuboresha na kukuza fikra za kijasiriamali
- Kufikia ubunifu ambao haujatumika bado katika kutatua matatizo kwa nyenzo zinazoendelea kubadilika
- Kujenga uthabiti katika jamii & uongozi duniani
-

**Kwanini** – Kama miaka 8 ya mwanzoni huwa inajenga msingi wa baada wa kujifunza, afya na mafanikio ya mtoto! Je, kwanini shirika hili lisihusishe kujitambua kama jamii, ili kuwapa watoto mazingira salama kwa ajili ya kukua na kuelekea katika utu uzima?

Programu hii imetengenezwa ili kutoa rasilimali kwa jamii, familia ambazo hazina kwa ajili ya kuwezesha ukuaji wa mtoto kuelekea utu uzima na kukuza ufahamu katika mambo yafuatayo.

1. Malezi ya mtoto na mifumo, ufahamu-binafsi, ongezeko lausalama wa kiuchumi na kijamii, kuhifadhi matarajio ya kujitambua..

**Nani** – Kila mtu anaweza kuongoza katika kufikia maono yake duniani, kama nyenzu muhimu zikitolewa kwake mapema. Programu yetu ni kwa vijana wote kati ya umri wa miaka 8-30 na zaidi, kwa sababu tunakuza

    1. Kujiajiri & kufanya miradi na kujifunza ujasiriamali
    2. Ufahamu wa sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM)
    3. Uwezo binafsi na wa vikundi wa kutatua matatizo

**Kivipi –** Tunawezesha ubunifu wa kijana kama mtoa maamuzi kwa

1. Kuwekeza katika ufahamu mapema – kuelewa hofu, kukuza uwezo, na kukumbatia upekee
    1. Kutengeneza mtandao wenye afya na tija kuelekea katika utu uzima
    2. Kuendelea kugundua nyenzo za kuboresha na kuvuka vizuizi, kukabiliana navyo na kukua
    3. Kutumia mambo yaliyofundishwa mtu-na-mtu katika huduma za kijamii

**Je, uko tayari kuongoza na kupata ubunifu wako?** Kamilisha fomu moja wapo ambayo inakufaa.
Mshirika wa Jamii|Nyumbani/Wazazi | Waalimu/Waliojitolea/Wajasiriamali|Waalimu wa Wataalamu/Wamiliki wa Biashara |Wazungumzaji

## I. Uwekezaji

Tunasimamia matukio kwa watu walio na miaka 8-18 | 18-30 kila mwaka na kuwekeza katika mawazo ya kibunifu.

**Viongozi wenye miaka 8- 18**
- Jumla ya zawadi $500
- Mwezi 1 wa mafunzo & kuelekezwa
- Tukio la Mwaka
  - Novemba (Marekani watahudhuria kwa njia ya mtandao)(Nchi zingine wanaweza kufika ana kwa ana au kwa njia ya mtandao)

**Viongozi wenye miaka 18-30**
- Jumla ya zawadi ya $5,000 - 25,000 (Miezi 3 ya mafunzo/Kuelekezwa Huduma za Ushauri)
- Tukio la Mwaka - wiki 2 (Nchi itatangazwa mwisho wa Novemba)
  - Uzoefu wa duniani kwa 18-30
  - Kusafiri Januari au kuhudhuria tukio kwa njia ya mtandao

## II. Uchaguzi wa mawazo

Tunachukua mawazo kulingana na vitu hivi hapo chini, hata hivyo, sio tu hivi katika hii orodha pekee.

**Timu**
- Ufanisi Mawasiliano, Usimamiaji wa Muda, Heshima, Kuaminika Uhusiano
- Uongozi Uwajibikaji, masomo, kuomba msaada

**Wazo**
- Kuishi & kuelezea kwanini - hadithi yako ni ya muhimu
- Je, kila mtu anaweza kufaidika na hadithi/wazo lako?

**Athari**
- Je, inafaa kila mtu?
- ni kwanini na kwa namna gani unajiona wewe au mtu mwingine akifundisha timu yako?
- Muunganiko zaidi ya hadithi yako (je, kuna mtu mwingine anaweza kuiboresha)

TazamasehemuGkwa ajili ya muongozo wa kusaidia timu yako kujitathmini wenyewe. Tazamamfano wa pitch - sehemu C

- Kwanini ulichagua wazo hili? | Ni kwanini hili ni wazo zuri, kwa sasa? Nini kimebadilika duniani?
- Ni kwanini hili halijafanyika miaka kadhaa nyuma? | Ni jambo gani unalojivunia zaidi kulikamilisha?
- Umefika mbali kiasi gani? Kizuizi chako kikuu ni kipi? | Washindani wako ni kina nani? Nani ni tishio kubwa zaidi? | Unafahamu jambo gani ambalo washindani wako hawalifahamu? | Utatengenezaje pesa?
- Hatari kubwa ni ipi? Kama ukifeli, nini inaweza kuwa ni sababu? Ni nini kinatakiwa kwenda sawa ili fanikiwe?
- Unahitaji msaada gani zaidi? | Unaathirije ulimwengu kwa namna chanya?

## III. Chagua majaji kwa ajili ya mawazo

Tunatafuta wawakilishi wenye miaka 18-80 duniani kote kulingana na vitu vifuatavyo na zaidi.

**Wadhamini/Wafadhili wote**
- Eneo la kufanyia tukio
- Michango ya chakula
- Waalimu wa Chuo Kikuu
- Washiidi wa ndani katika biashara
- Nyumba za wageni & safari
- Hospitali
- Shule/vyuo vikuu vya eneo hilo na vya kitaifa
- Waalimu
- Maeneo ya kufanyia kazi
- Wafadhili wa Visa & safari

**Pesa & Wanaowekeza Muda**
- Ufadhili kwa ajili ya usafiri
- Wataalamu wa Chuo & Viwanda
- Huduma za afya, Nyumba ya wageni & chakula
- Waalimu na wakufunzi wa uwasilishaji (presentation)
- Wataalamu wa STEM
- Washindi wa ndani
- Kukusanya ufadhili binafsi na kupitia marafiki
- Waalimu
- Maeneo ya kufanyia kazi

**Rasilimali & wafadhili wa Maendeleo**
- Kila tunachoweza kukipata chenye umuhimu
- Rasilimali za STEM
- Familia, marafiki, na zaidi
- Serikali za Mtaa, Kitaifa na ya Shirikisho
- Rasilimali za kusafiria
- Uwekezaji wa muda mrefu katika jamii
- Kushauriwa na Kuelekezwa
- Chochote kinachohitaji tukusanyike
- Waalimu
- Maeneo ya kufanyia kazi

## IV. Faida kwa Majaji

- Fursa ya kupata fedha za kusafiria na timu yako ya uongozi ya kitaifa kila mwaka
- Uwezo wa kuajiri na kujihusisha na maendeleo ya vijana
- Kuzungumza, kufundisha viongozi/wazazi wengine
- Kuwa mshauri wa bodi katika nchi yako na duniani
- Mafunzo ya mwaka juu ya uwekezaji wa eneo lako na mabadiliko
- Kujenga mahusiano muhimu ili kukusaidia kukua, kadri unavyozidi kubadili maisha ya wengi kwa kutumia maarifa yako
  - Tunatafuta angalau wawakilishi sita wan chi kwa kila nchi
  - Uwezo wa kuzungumza Kiingereza ni muhimu, japo kuwa sio lazima kama utakuwa tayari kujifunza

## V. Maandalizi kidunia & Ratiba

Mnamo Januari, mawazo na makundi yote yatachaguliwa ili kushiriki.

**Viongozi wa Kitaifa — Miaka 8-18**

**Novemba**

Kukamilisha waalimu/wanafunzi wa miradi ya kitaifa pamoja na uwekezaji

**Septemba–Novemba**

Kufungua na kufunga kwa maombi ya washirika, waalimu na wanafunzi

**Viongozi Kidunia — Miaka 18-30**

**Desemba**

Miradi yote ya kimataifa inachaguliwa na taarifa za safari zinatolewa

**Januari**

Uwekezaji wote kimataifa unafanyika, mabalozi wa Mataifa na wa Kimataifa wanachaguliwa

## VI. Maeneo ya Matukio ya Kidunia

Kwa muda huu, matukio yetu ya kidunia yatafanyika ndani ya **Rwanda, Haiti au Kwa njia ya mtandao kwa washiriki walio na umri wa miaka 18-30**, isipokuwa tu kama tukiwataarifu washirika miezi sita kabla kama kuna mabadiliko yoyote. Matukio yote ya walio na miaka 8-17 itafanyika kwa njia ya mtandao kwa Marekani na ana kwa ana au kwa njia ya mtandao kwa washiriki wa nchi zingine.

## VII. Eneo la kazi

Tunakwenda mahali ambapo tunaweza kushirikiana na vijana. Kwa sasa tuna wadau katika nchi zifuatazo.

| Afrika | |
|---|---|
| Rwanda, Tanzania \| Tunafanya kazi kwa njia ya mtandao na kuna timu iliyopo eneo hili | Woc@womenonchange.org \| 202-656-0077 (WhatsApp) \| wocLexima (Skype) |

| Caribbean/Amerika Kusini | |
|---|---|
| Haiti \| Tunafanya kazi kwa njia ya mtandao na kuna timu iliyopo eneo hili | Woc@womenonchange.org \| 202-656-0077 (WhatsApp) \| wocLexima (Skype) |

| Marekani | |
|---|---|
| Ofisi ya Mtandaoni \| Tunafanya kazi kwa njia ya mtandao na katika eneo hili kadri inavyohitajika | Woc@womenonchange.org \| 202-656-0077 (WhatsApp) \| wocLexima (Skype) |

**Utatupata mtandaoni kupitia** - WoC on youtube, facebooknatwitter.

## 2. Maswali ya mara kwa mara (FAQs) na Vidokezo

Sehemu hii katika nyaraka hii inatoa taarifa zaidi juu ya programu ya Ongoza na Pata Kipato au Lead and Earn. Pamoja na viungo(links) na maandishi yanayopatikana mtandaoni kukusaidia kuelewa zaidi, namna ya kujiandaa au kuweka mipango yako mwenyewe kabla ya mafunzo yetu, au kushiriki katika programu.

### I. Ninajiungaje au kuwa mshirika katika programu hii?

Tembelea tovuti yetuhttps://womenonchange.orgna ujaze maombi.

### II. Tunatoa nini kwa washirika?

Sisi ni washirika imara wa kukabiliana na changamoto za kijamii na kiuchumi katika ngazi ya chini kabisa, kwa kuwajenga watu wanaotakiwa kuongoza – ambao ni vijana. Hivi ni baadhi ya vitu tunavyotoa kwa washirika.

- Mafunzo ya Kutunga Mawazo & Kujitambua | Uwekezaji&maendele ya ujasiriamali |Usimamizi wa Programu
- Uhamasishaji wa Tamaduni | Kuunganisha Sekta Mbalimbali | Kutafsiri lugha & wakalimani & kuchapisha
- Usimamizi wa ufundishaji & Kuajiri | Utayari wa chuo na ufundishaji | Huduma za kisheria na biashara zingine
- Mafunzo ya watoto na ya usalama | Mipango ya kusafiri duniani

Japokuwa mabadiliko yote yanayodumu huwa yanaanza ndani yako. Mtandao wetu wa kimataifa unaweza kukupa huduma yoyote ile ambayo unadhani unaweza kuihitaji ikiwa ni pamoja na zifuatazo:

Wawekezaji (Angel investors) | wajasiriamali| NGO |Wawekezaji wa Kibepari (Venture Capitalist )| serikali | mashirika | wazazi | taasisi za K-12| washauri – wa umri wowote | vyuo/vyuo vikuu | makampuni | waalimu katika ngazi zote | washauri|wataalamu wa mada fulani | Waponyaji | wasafiri wa duniani | wasanii | watu wa aina mbalimbali waliojitolea | Washauri wa mambo ya kisheria | wataalamu wa STEM | Mabingwa wa mabadiliko

### III. Mahitaji ya kuwa mshirika

Eneo la kufanyia tukio | Ufahamu juu ya jamii |Upatikanaji wa simu na intaneti, itakapohitajika | Uwezo wa kufuata miongozo ya programu ya WoC | Wewe au mtu mwingine anaweza kuongea Kiingereza au anaweza kutafsiri programu yetu kwenda katika lugha yako | Anaweza kuhudumia angalau vijana 10-20 kila mwezi kwa muda wa mafunzo wa mpaka masaa 20.

### IV. Tunatafuta washirika wa aina gani?

Watu wenye miaka 18 na kuendelea | Wazazi | Viongozi wa jamii na mashirika | Viongozi wa biashara – za ndani, mikoani – haswa katika maeneo yanayojihusisha na elimu | Wajasiriamali walioguswa | wajasiriamali – wauzaji wadogo wadogo | Watoa elimu Pre-K-12

### V. Tunawawezeshaje washirika?

Programu inahitaji taaluma kadhaa ili kufanikiwa. Kama upo katika nchi ambayo hakuna imani kwa taasisi, watu, na ni vigumu kusimamia au kuokoa muda. Tumeungana na watu wa ndani ili kukusaidia kuokoa (Tazama sehemu E)na kisha kutengeneza muundo kwa ajili yako mwenyewe. Tunakumbatia ushirika unaowezesha kuondoa changamoto

Punde tu baada ya kufanya maamuzi ya kushirikiana na sisi, viongozi wetu wa eneo lako watafanya kazi na wewe kuhakikisha kwamba una nyenzo zote unazozihitaji ili kufanikiwa.

**Nidhamu ya kifedha ni muhimu**. Modeli ya kuhifadhi kama kikundi haitumiki Marekani, sababu benki zinapatikana kwa wingi kukuhakikishia unahifadhi vizuri.

**Ufadhili**unategemea na majukumu ya uongozi na huduma za ufundishaji za watu waliopo katika jamii na wazazi. Kikundi cha mafunzo kimejikita katika kufundisha kujitambua kwa watoto na kutoa nafasi ya kufikiria, kushirikiana pamoja, na kukosea pia.

- Tunazidisha hifadhi ya mwaka ya familia mara mbili kwenda katika ushiriki wa wasichana wa miaka 8-18 katika programu katika nchi zilizochaguliwa
- Tunawezesha familia, ambazo zinachukua wajibu kuelewa changamoto zinazowaathiri wao na watoto wao na kuzivuka, kwa kuruhusu ufundishwaji. Mafunzo haya yanajikita zaidi katika elimu ya hisabati na mawazo ya miradi. Tazama mfano wa elimu ya hisabati. tazama sehemu C:

**Uchaguzi wa waalimu & wanafunzi** – Tazama maombi ya mtandaoni. Tunaangalia vitu vifuatavyo kutoka katika waalimu

- Waalimu wote watakaokidhi vigezo watachaguliwa kutokana na wazo au tatizo wanalotaka kulitatua
- Wanakubali kufanyiwa uchunguzi kiusalama (security background check) kama wakichaguliwa kuwa waalimu wa watoto wa miaka 8-18, watakapohitajika

**Maandalizi Kimataifa**–Waalimu 18-30 watahitaji kuweka akilini mwao mambo haya yafuatayo, kama wakiamua kuchagua kushiriki katika safari hii ya ujasiriamali.

- Uwezo wa kusafiri, mfano. nyaraka za nchi zinazohitajika | Uelewa wa kawaida wa Kiingereza, hata hivyo, sio lazima | uwezo wa kufanya kazi na wengine | Uwezo wa kuiwakilisha nchi na mawazo yao mbele ya ulimwengu

## VIII. Je, tunatoza pesa kufundisha washirika?

Ni bure kushiriki programu hii kwa vijana wenye umri wa miaka 8-30. Kama ungependa tukufundishe kutumia programu hii ndani ya jamii yako au mwalimu amfundishe mtoto wako, tunatoza gharama ambazo zitakuwa zinahusiana na mafunzo. Mchanganuo wa gharama za mafunzokwa mfano:

**Gharama ya ada - $15x1**
- Safari ya Ndani au ya Kimataifa
- Kutafsiri
- WiFi
- Chakula
- Nyumba ya wageni


**Mchango wa Programu Yako - $35 x 5(timu) unaenda katika mafunzo yako au mradi.**
- Uwekezaji wa wazo
- Usafiri
- Kuchapisha nyaraka za pdf
- software

**Mafunzo yanakufundisha**

1. Namna ya kuitekeleza programu hii ndani ya eneo lako au kitaifa
2. Kufanya ujasiriamali na kutekeleza programu hii katika jamii yako
3. Pia tunakufundisha kugundua bei katika jamii yako, kama una mpango wa kutoza pesa kwa ajili ya programu yako
   a. Sehemu ya bei inaenda katika gharama za uendeshaji na nyingine katika wazo lako
   b. Unajifunza namna programu inavyofanya kazi kwa kuwekeza pesa katika wazo lililogundulika
   c. Tunapendekeza washiriki 50 kwa kila eneo kwa mafunzo ili kuokoa gharama

## IX. Uanachama & mafunzo ya WoC

**Punguzo la Uanachama** – Kama wewe ni mfadhili, inamaanisha kwamba robo ya ufadhili unaenda WoC. Kwa watu ambao sio wanachama, tuna programu kwa watu wenye umri wa miaka 18-40, tafadhali tembeleawww.triventures.today.





**Mchango wa mwaka & Faida zake**

## X. Malipo ya mtandaoni

Malipo yote yanapokelewa mtandaoni katika tovuti yetuna tunashirikiana na watu eneo lako kufanya malipo ya watu binafsi mtandaoni kwa usalama na kupokea risiti, maeneo ambayo benki haipo karibu. Tunalipia ada za kufanyia malipo ya washirika wetu kwa yoyote ambaye atakuwa hana akaunti ya benki.

## XI. Ratiba ya Mafunzo

Tunashirikiana kwa ukaribu na washirika wa ndani, pale inapohitajika katika mafunzo katika miezi ifuatayo.




## VI. Ili kutekeleza programu hii, nifanye nini?

Jitahidi usimuache mtu yoyote nje kwa sababu ya mambo ambayo wewe inawezekana haukubaliani nayo, tafadhali kuwa kiongozi anayejumuisha watu kwa kadri utakavyoweza. Amua makundi yako, mfano makundi yanayoendana zaidi na jamii yako. Kwa mfano

- Umri (miaka 3-5, 6-10, 11-15- 16-21 n.k., | Miradi | Masuala | Mawazo | Jinsia | Changamoto binafsi na zaidi.

## VII. Amua muundo wa timu yako

Tunapendekeza usiwe na zaidi ya timu 4, au watu 20 wanaoshiriki kila mwezi kwa maandalizi. Kwa mfano, unaweza kuwa na shule 20 katika jamii yako zinazoshiriki programu hii. Kila mwezi, tunapendekeza kila mshirika apokee

watu mpaka 20 na sio chini ya 10 kwa kila darasa kwa kila saa moja. Programu hii inashirikisha watu na inahitaji watu kuunda makundi na kushirikiana. Kama ukiamua kufanya kazi mwenyewe au katika timu kubwa ya watu 3 mpaka 5, haitakuwa na ufanisi. Tazama faida ya kufanya kazi katika timu kwenye kipengele cha rasirimali.

Muundo huu chini wa timu unaweza kutumika kama mfano wa namna unavyoweza kutengeneza programu yako. Ni mfano tu. Kikundi chako cha hifadhi hakitegemei programu yetu.




**VIII. Miongozo ya kufanya kazi kama timu**

**Miongozo ya makundi**>>
http://employees.oneonta.edu/vomsaaw/w/psy220/files/GroupWorkGuidelines.htm

| **Heshimu kila mmoja wenu.** | **Kila mwanachama wa kikundi anatakiwa kufanya kiwango sawa cha kazi.** | **Kikundi chako hakitakiwi kuwa na uelewa sawa wa malengo yanayohitajika kufikiwa.** | **Kuwa tayari kupokea mabadiliko.** | **Mawasiliano fanisi.** | **Usimamizi wa Muda.** |
|---|---|---|---|---|---|
| - Heshimu mawazo ya kila mtu<br>- Heshimu wanachama wa kundi lingine<br>- Msikatishane ninyi kwa ninyi<br>- Mtazamo wa kila mtu ni wa thamani<br>- Kuweni wakweli baina yenu | - Kila mtu ashiriki katika kuwajibika kwenye kazi<br>- Usichukue kazi ya mtu na usikubali wengine wachukue ya wengine | - Saidianeni muweze kuelewa dhana(concepts) zote | - Kuwa tayari kushirikiana na wengine katika mawazo yao<br>- Kuwa na mawazo wazi<br>- Pigeni kura pale ambapo hamkubaliani | - Hakikisha kwamba kila mtu anaweza kuzungumza juu ya mawazo na matatizo yake<br>- Toa mawazo yako bila kujali yako "nje" kwa kiwango gani<br>- Sikiliza kwa umakini<br>- Usiwe mkosoaji | - Fika ndani ya muda katika vikao vyote vya kikundi<br>- Kuwa tayari kupokea mabadiliko ya muda wa mkutano<br>- Weka umakini katika kazi husika (punguza mazungumzo yasiyohusiana na tukio) |


### IX. Tambua muundo wako wa ndani wa ufundishaji

Utakapofika muda wa kufadhili mtoto yoyote, unatakiwa kumuandikisha kwa ajili ya mafunzo kabla, sio tu pale watakapokuwa tayari kushiriki kimataifa. Baada ya kumuandikisha mtoto wako kushiriki katika mafunzo ya kikundi au kuwa mwalimu. Wazazi wote na mtoto ni lazima wahudhurie vikao vya kuhifadhi na kusimamia mafunzo ambayo yatakuwa yakifanyika.

Tunapendekeza wazazi washikiane na kubadilishana kila wiki kusimamia mafunzo, hii itahakikisha kwamba mtoto wako anapata kile anachokihitaji ili kufanikiwa.

- Mzazi au mtu yeyote, ambaye ni mlezi anaweza kumuandikisha mtoto kwa ajili ya mafunzo, baada ya kujiunga au kutengeneza kikundi cha uihifandhi
- Watoto, ambao hawatakuwa na mlezi au mwanafamilia kuwawakilisha, na wako chini ya miaka 18 wanaweza kujiwakilisha wenyewe katika programu ya mafunzo

Hata hivyo,kama mtoto wako akifika katika ngazi ya uongozi wa kitaifa, mafunzo yatamsaidia kufanya vyema shuleni, kupata ujuzi wa kazi na ujasiriamali ndani ya muda mfupi. Waalimu na wanafunzi wote pamoja wanafudhu kupokea mchango wa ufadhili. Tazama Sehemu F kupata miongozo ya ufundishaji.




---





### X. Tazama Waalimu

Kwa madhumuni ya ufadhili (washirika nje ya Marekani), tuna imani tu na timu ya eneo la ndani, wazazi, familia na mtoto kama kiongozi awe mkweli katika mchakato wa kuhifadhi kumbukumbu ambazo zitakuwa zikitumwa kila mwezi. Nyongeza, tutathibitisha, kama mafunzo yanatolewa kwa kulingana na vifuatavyo:

- Idadi ya masaa yaliyotolewa na kila mtu kwa sababu inaonyesha maendeleo ya mtoto katika ngazi ya kitaifa. Tazamasehemu Bna katika fomu ya mafunzo kwa programu yako mwenyewe, tunaweza pia kukutumia katika barua pepe.

**XI. Kuanza**




**Bainisha mradi wako wa kijamii, nani aliye bora atakayeongoza mabadiliko kimataifa kila mwezi**

Hapo juu ni mfano wa washirika wote – ni muhimu sana jamii yako ishirikishwe katika mchakato ili kufanikiwa. Tunapendekeza kubadilisha viongozi wote kila mwezi ili kila mtu ashiriki na kuona mtindo tofauti wa kufanya kazi. Shirikisha jamii yako iweze kushiriki katika kila ngazi, pale inapowezekana.
Kila wazo litakalochaguliwa linatakiwa kuwasilishwa kwa wenginem wazazi, jamii, ndani na kuboresha wazo zaidi, ya wale waliolileta. Kila robo muda, kugundua wazo bora la kushindanishwa kitaifa na kidunia. Vidokezo vya uchaguzi wa mawazo ya uongozi kitaifa.


- Toa fursa kwa kila mtoto katika jamii yako kujiunga katika programu ya kila mwezi
- Kila robo muda, chagua viongozi wako wa juu kwa ajili ya kuwaonyesha katika eneo lako
- Endelea kushirikisha watoto wapya kadri unavyozidi kuendelea kufundisha wale ulionao
- Tumia ufundishaji wa kila mmoja wao kwa wao kumsaidia kila mtoto kuweza kukuza kipaji chake kutekeleza miradi ya ndani, pamoja na kuongoza programu pia
- Hitaji la umri katika kuongoza programu katika jamii yako – tunapendekeza umri wa miaka 18 au zaidi kwa wale wenye miaka 0-17.

**XII. Vidokezo vya Kujiandaa-Kabla**

Tazamasehemu E kupata **muongozo wa programu ya kuhifadhi**, kama hauna mpango wa kuhifadhi katika nyumba au jamii yako, tengeneza wa kwako. https://welldoing.org/article/5-key-benefits-teamwork-and-collaboration

Ni rahisi kwa timu yako, kama itachaguliwa kutoka katika kikundi cha kuhifadhi au programu nyingine ya kuhifadhi ya ndani, au kama unajua ujuzi wao binafsi katika kukamilisha mambo. Tunakushauri uwe huru sana katika kuchagua timu yako, inasaidia kushirikisha watu tofauti, kuboresha ukuaji na kujitambua. Wakati mwingine, vitu rahisi havitusaidii kukua. Tunapendekeza sifa zifuatazo ili kupata timu bora.

- Kuvutiwa katika matatizo makubwa | Bora katika kusimamia muda na kutunza ahadi zao | Sio muoga katika kuchukua kazi na kujieleza pale anapokutana na wakati mgumu
- Sasa, ili kuanza, anza na zoezi hili dogo. Mwambie kila mtu katika timu afikirie na kuja na vitu viwili vya muhimu – mawazo yao bora ya uwekezaji. Tazama jinsi ilivyoonyeshwa hapo chini.




**Ongoza kwa madhaifu yako, uoga, ili kugundua ujuzi mpya, kukuza nguvu ulizonazo kuacha athari.**

### XIII. Mradi & wazo

Mawazo yanaweza kuwa ni ya aina mbalimbali kama vile kupanda miti, vituo vya juisi ya limao, kutengeneza nguo, kupiga picha, kufundisha, kuandaa mapishi, sanaa, kufundisha wasichana na wavulana namna ya kushonda, uwanja wa kucheza watoto, kumuelimisha nesi namna ya kuhudumia jamii yako, kuongeza ufahamu juu ya mabadiliko ya hali ya hewa, kujenga shule, barabara, kliniki na zaidi, tazama sehemu ya changamoto kwa msaada wa mawazo. Hakuna ukomo wa ubunifu wako!

**Lengo lako ni kufanya jamii yako ijitegemee**, kwa kutumia vitu ambavyo vipo tayari, na vinafanya kazi katika jamii ili kufanikisha hilo. Kabla haujaanza, hakikisha unajua ni nini hasa unachohitaji, na ujuzi ambao unakosekana na uliopo. Kwa mfano, unataka kusaidia jamii kukuza ujuzi fulani? Kubadilisha namna ya kufikiria katika kutatua matatizo? Au kutengeneza fursa mpya?

### XIV. Wazo gani au biashara gani ni kubwa?

Hauwezi kuwa na biashara bila kuwa na wazo bora. Wazo bora siku zote linaanza kwa kutaka kuona jambo tofauti au jambo bora zaidi kwa mtu zaidi ya mmoja. Women on Change, kampuni ambayo unalipia kupata huduma zako za simu, simu yako ya mkononi, chakula kilichofungwa unachokula, vyote wakati fulani vilikuwa ni mawazo tu. Habari njema ni kwamba katika nchi ambazo kuna uhitaji mkubwa, unaweza kutengeneza kitu chochote salama kwa ajili ya watu.

### XV. Kwanini kufikiria kunasaidia?

Jikite katika kuwa na fikra za ukuaji (growth mindset)https://www.edglossary.org/growth-mindset/
Kufikiria (brainstorming) ni kuelewa watu katika timu ako na nguvu ya ubunifu wao katika kutatua matatizo, wote mnatafuta namna ya kutatua matatizo katika jamii yenu.

Tunapendekeza zoezi lifuatalo kwa ajili ya kuchangamka:

- Andika vitu viwili ambavyo siku zote umekuwa ukivitaka, kwa mfano, kama ndoto yako ni kuwa na pasi ya kusafiria duniani kote na kwenda popote pale au kujifunza lugha mpya. Hakikisha vitu hivi viwili view ni vitu vinavyoweza kuonekana kwako na sababu za kwanini ni muhimu kwako na kwa wengine
- Kila timu inatakiwa kuchukua muda na kuandika mawazo mengi kadri inavyowezekana
  - Siku zote pumzika katikati ya kazi, baada ya dakika 45. Tazama sehemu yenye vidokezo ya kufikiria:

### XVI. Ushirikiano

Fahamu nguvu ya kushirikiana ili kuinua jamii yako, sio tu wewe peke yako. Tunapendekeza yafuatayo baada ya wanachama wote watano katika timu yako wakijiunga.

- Andika mawazo 2 makubwa ambayo kila mtu anataka kuyakabili
- Jadilini mawazo kwa ukweli na yasimamie!
- Lengo lako ni kuwashawishi wanachama wa timu yako kwamba wazo lako ni bora, kwa kuwaonyesha jinsi lilivyo la ushindi na linavyoweza kuwa na athari endelevu
- Tazama boksi la njano juu litakalokusaidia kujua wazo gani ni zuri
- Ukimaliza kuchagua wazo lako kuu, liwasilishe kwenye timu yako, kuona kama litapendwa na jamii na maswali ya kutafakari
- Wewe ni kiongozi unayeongoza mabadiliko katika maisha ya watu na kubadili dunia. Fikiria kwa upana mkubwa!

### XVII. Mawazo yaliyochaguliwa

Haijalishi wazo lako ni bora kiasi gani, timu yako, jamii, wadau wan je, na wawekezaji ni lazima waungane na wazo moja kwa wakati mmoja. Kumbuka, pamoja tunaweza kwenda mbali. Sasa kwa sababu umepata suluhisho la tatizo unalotaka kulitatua. Badilika kutokana na hali. Wazo lako linaweza kuchukua uelekeo mwingine au kubadilika kabisa, kadri unavyozidi kuzama ndani katika kupata utatuzi.

### XVIII. Kiasi cha uwekezaji

Kiasi unachowekeza katika mradi wako kinategemea na jamii yako na tatizo unalotaka kutatua. Unatakiwa kuzingatia gharama zitakazokuwezesha kuendelea kufanyia kazi lengo lako na kikundi cha rika la watu unaofanya nao kazi pia. Tutafanya warsha na viongozi wa ndani ili kukusaidia kugundua baadhi ya gharama hizi. Pia tunapendekeza usiondoke katika kundi la kuhifadhi pesa, kama ukichagua kutokujiunga na programu hii baada ya mwezi. Unaweza kujiunga na programu mwezi kwa mwezi kwa kadri inavyohitajika. Huu ni uwekezaji wa muda mrefu, kama unatamani kufanya mabadiliko halisi, ujasiri ni muhimu.

### XIX. Mipango na kujua ujuzi

Unatakiwa kujua baadhi ya maeneo ya nguvu katika timu yako na maeneo ya kufanyia maboresho kwa sasa. Kila mmoja sasa atagundua namna atakavyokabiliana na tatizo hili ambayo ni ya kipekee katika jamii yako. Hapa ndipo ufundishwaji, kuelekezwa na ujuzi au msaada mwingine unapohitajika. Tunapendekeza yafuatayo ili kurahisisha mipango yako.

- Gundua maarifa makuu mawili ambayo unaweza kuyatumia au kujifunza kutatua tatizo hili na kuyajadili na timu yako
- Kisha chagua jambo moja ambalo unaweza kulifanya vizuri na unajua unaliweza sana na uendelee nalo
    - Tafuta mengine ambayo hauko vizuri nayo na namna wenzako katika timu wanaweza kukusaidia kuwa bora zaidi
- Kutokana na zoezi hili, mkabidhi kila mwanachama katika kundi kazi katika wazo hili
- Kwa chochote ambacho kinakosekana katika kutatua tatizo, kitafute nje ya timu yako ya watu watano
- Kumbuka kwamba wewe ni sehemu ya jamii, kamwe hauko peke yako! Utahitajika kushawishi jamii ili kushinda zawadi za kitaifa na kidunia

**Vidokezo kwa timu:**
https://www.thinkwithgoogle.com/intl/en-gb/marketing-resources/content-marketing/five-dynamics-effective-team/ | Kuchagua vidokezo vya timu - https://uwaterloo.ca/centre-for-teaching-excellence/teaching-resources/teaching-tips/tips-students/being-part-team/teamwork-skills-being-effective-group-member

### XX. Changanua&Hakikisha wazo

Wakati wa mipango, lengo lako ni kuelewa uwezekano uliopo wa kutatua tatizo hili, ambalo linaweza kuwa kampuni ya kidunia. Unakwenda kugundua katika Uhakiki, kama wazo ni tatizo halisi na kama unaweza kulikabili.

Timu inaamua kama unaweza kukabiliana na wazo hili kwa msaada wao, mfano. Jamii yako ina ukubwa kiasi gani? Kama ndiyo, endelea na, kama sivyo, kumbuk kwamba kuna mawazo mengine 9 makubwa ya kuyarudia. Kumbuka kurudi kutaza katika sehemu ya nini kinachofanya wazo kuwa kubwa. Moja ya mambo ya kuyafikiria ni kuweka watu katikati ya wazo lako.

- Ifanye jamii kuwa timu, mteja na jaji ili kuendea kujifunza namna ya kuboresha wazo hili
- Tafuta ni rasilimali kiasi gani kila mmoja wenu atachangia, na ufadhili mwingine wowote unaohitajika
- Fikiria juu ya namna, nani atakayeweza kuleta rasilimali za ziada katika timu yako – unaangalia muda, akili, pesa, ushawishi na zaidi

### XXI. Kutangaza & Kuuza wazo

Tutagusia hili wakati wa mafunzo yetu kwa kutumia Ubora wetu, Udhaifu, Fursa na uchambuzi wa Hatari (SWOT), ambayo unaweza kuifanya hata wewe binafsi. Hapa ndipo unapofanya maamuzi, ni kina nani ni wateja wako na kipimo cha kupima matokeo? Mahusiano mapya ni muhimu pia. Je, bidhaa inaweza kujiuza yenyewe au unahitaji watu wa kufanya hivyo? **Tazama vidokezo sehemu hii chini.**Bonyeza hapa kupata vidokezo

Ratiba ya muda ni muhimu kukusaidia kupangilia na kufuatilia malengo yako. Tunatumia ratiba ya programu kuelewa ni nini tunahitajika kukifanya katika ngazi ya uongozi kitaifa na kidunia. Tunapendekeza ufanye hivo kwa programu ya uongozi ya ndani na ya kimkoa.

### XXII. Ninajipangaje kwa ajili ya programu yangu (ratiba ba Bajeti)?

https://www.workzone.com/blog/microsoft-project-alternatives/

Jenga ratiba – tunakupitisha katika hili wakati wa mafunzo, tutakapoomwa.
Bajeti- Progamu hii ni jaribio lako la kwanza la ujasiriamali. Tutakupitisha katika kutgengeneza bajeti.

### XXIII. Nitekeleze vipi programu hii?

Ili kuokoa muda na gharama, usitume maombi ya mafunzo, mpaka utakapokuwa umekamilisha vitu hivi juu. Kabla ya kufanya kazi na washirika wote , kamilisha **fomu yetu ya washirika** | Fomu ya Mshirika wa Kijamii |Nyumba/Wazazi

Tunafanya kazi kubwa kupata taarifa nyingi juu ya mpango wako wa kutekeleza programu hii. Utafanya kazi na mratibu wan chi husika ili kuanza kwa kutumia nakala halisi zilizochapishwa.

- Fahamu wazo lako & utayari wa kujifunza
    - Timu na muundo uliopo wa ndani | Programu imekaaje katika jamii yako?
    - Vitu tunavyoweza kuvitoa | Muda wa kutekelezwa | Washiriki wa ndani na eneo
    - Mahitaji ya lugha | demografia | Bajeti na zaidi

**Baada ya kuchagua kushiriki** na wewe, tunatuma Hati ya Makubaliano au Memorandum of Understanding (MOU) na kuweka ratiba ya mafunzo ya programu yako ya ndani.

**Kamilisha mipangilio yako** ni muhimu kabla ya wakati, na tunasaidia kuthibitisha mahitaji hayo juu.

Tunawaleta washirika kukufundisha, itakapohitajika, hata hivyo, tunakabiliana na timu za ndani zifuatazo:

- Mafunzo yanafanyika mtandaoni na ana kwa ana
    - Kuwekeza katika wazo lako | Programu ya mafunzo na kuhifadhi
    - Kuelekezwa & kufundishwa | Tiba & ushauri
    - Pitia katika mchakato wa kutengeneza na kuwekeza muda | Rasilimali zinahitajika

### XXIV. Ujasiriamali ni Nini, Ushauri, Kufundisha

Programu hii, makundi ya watu wa miaka 8-30, ambao wanaweza kushiriki katika ngazi ya kitaifa na kidunia wanapokea huduma zifuatazo. Hiki ni kitu ambacho tunaweza kukufundisha katika mafunzo yetu, unapokuwa ni mshirika pia.

1. Ujasiriamali – "Hali ya kuanzisha biashara moja au zaidi, kuchukua hatari ya kifedha kwa matarajio ya kupata faida."
   - Unahitaji uzoefu kujifunza na kuwezesha mtandao wa wawezeshaji ili kufanikiwa
   - Inahitaji ujasiri na uwezo wa kubaki katika mstari, kupenda, muda na kuwa na usawa
1. Ushauri (mentorship) – "Kipindi ambacho mtu anapokea muongozo kutoka kwa mwalimu."
   - Inahitaji utayari wa kutumia nyenzo na kuwa wakweli juu ya kile unachokutana nacho peke yako au kama kikundi
   - Inahitaji ujasiri na uwezo kuvuka changamoto na kubadili jambo, huku ukishirikisha taarifa za siri, kupokea mrejesho, huruma bila unyanyasaji au kumtumia mtu
1. Mafunzo (coaching) – "Ni kufungua uwezo wa mtu kukuza utendaji wao wenyewe"
   - Unachofanikiwa kupata ni utayari wa kugundua nini kilichopo ndani yako kukitumia wewe mwenyewe

### XXV. Ni Mafunzo, Uponyaji na Tiba gani zinatolewa?

Nyaraka hii inakupa rasilimali nyingi za kukusaidia kuelewa namna mishtuko (trauma) na tabia zinaweza kumuathiri kila mtu hasa watoto. Ukiwa mshirika, unapokea mafunzo kila mwaka kwa njia ya mtandao na pia ana kwa ana, kukiwa na watu wengi waliojiunga. Programu hii inahitaji kiwango cha kujitoa kutoka kwa mtoto, wazazi, jamii na viongozi wa ndani. Tazama sehemu ya 3 ya nyaraka hii kuona rasilimali.

- Mafunzo haya yamejikita katika kuelimisha jamii juu ya tabia zisizojulikana au imani za kihistoria ambazo zinaweza kuwa zinawazuia kukabiliana na matatizo, ikiwa ni pamoja na afya ya kiakili, njaa, mshtuko wa kihisia, manyanyaso, na zaidi
- Jamii zinakuja na changamoto ambazo wanakutana nazo binafsi ili kupata majibu kutoka kwa wataalamu.

### XXVI. Mafunzo yapi ya Biashara yanatolewa?

Tunafanya kazi duniani kote kutoa mafunzo kwa washirika wetu wote kila mwaka, kwa njia ya mtandao na ana kwa ana inapohitajika, kukuelekeza katika maeneo yanayohitaji msaada wa ziada ili kufanikiwa, utakapokuwa umegundua suluhisho la tatizo unalotaka kulitatua. Programu hii itakufanyia warsha kila mwaka katika nchi ambazo ni washirika wetu.Tazama sehemu Ikupata rasilimali za bure na za kulipia.

- Lengo la mafunzo ni kuwezesha wazo lako la kijasiriamali. Warsha hizi zitaandaliwa kulingana na changamoto ambazo mnapitia kama kikundi. Baada ya changamoto hizo kubainishwa, tunafanya kazi na waalimu katika nchi yako husika kukuwezesha kwa njia ya mtandao na uso kwa uso.

### XXVII. Utayari wa Chuo & Elimu

Wanafunzi katika programu yetu ya mafunzo wanakidhi vigezo na kuwa tayari kupata warsha mbili za chuo wakifanya kazi na waalimu na wataalamu. Warsha zinafanyika mtandaoni na uso kwa uso katika nchi zilizochaguliwa.

### XXVIII. Tunachukuaje waalimu katika programu yetu?

Viongozi wote wa ndani, ambao wanatamani kushiriki katika kuwezesha watoto chini ya miaka 18 wanapata msaada katika kupokea waalimu. Ambapo washirika hawataweza kutuma ombi kwa njia ya kielektroniki, watapata nakala ngumu kwa ajili ya kuzijaza na kuzikabidhi kwa timu yetu iliyopo eneo hilo. Kama waalimu wa kimataifa watakuwa wanahitajika, tunaweza kuchukua yoyote duniani kutokana na ombi husika.

**Tunachaguaji waalimu kwa programu ya kimataifa?**
Waalimu walio chini ya miaka 30 wanachaguliwa kwa mchakato sawa na ule wa kuchagua washirika. Wanapitia mafunzo tofauti, mchakato wa ukaguzi kama wajasiriamali wapya, na kupata fursa ya kuwa waalimu.
**Tunatoa wapi waalimu, na unawezaje kuwapata?**

- Vyuo vikuu vya taifa ndani ya Marekani | Bodi za vyuo na vyuo vikuu | Washirika wenye makampuni na NGO | Kupitia ujumbe wa maneno ya mdomo | Tovuti yetu na programu zetu | Mtandao wa wataalamu

**Maombi ya Waalimu**– Kutakuwa na waalimu 5-10 wanaosafiri kila mwaka kwa washirika waliotuma maombi, waalimu walioweza kupata mchango wa kulipia tiketi zao za ndege na washirika watatoa sehemu ya wao kukaa kwa usalama. Pia tutawezesha uchukuaji wa waalimu katika nchi yako husika, kama ukiwa ni mwanachama wa WoC. Maombi yote ni lazima yatumwe miezi mitatu kabla ya tarehe husika ya utekelezaji. Tunaweza kukupatia mkalimani wa kufanya kazi na timu yako.

### XXIX. Je, tunawalipa waalimu?

Sio wanafunzi wote wanaweza kugharamia au kutoa muda wao. Ndani ya Marekani, waalimu wetu ni kwa njia ya mtandao tu. Tunasaidia kuwa na waalimu bora, kwa kutoa fedha za usafiri na chakula pale inapohitajika. Tunashauri ufikirie hivyo pia katika programu ya uangalizi ndani ya jamii yako.

### XXX. Ni mafunzo gani & vitu gani vinavyotolewa

Tunawaongoza washirika katika mafunzo na kuwapa nyaraka, punde baada ya kugundua mahitaji ya programu yako. Taarifa zote hizi chini ni bure, ukijisajili katika mafunzo yetu. Waalimu wa mafunzo wanatokana na aina ya programu ambayo unaifanya, kwa kiwango cha chini kabisa tunahusisha yafuatayo:

- Uongozi unaowajibika| STEM Mentoring Hope –
    - Kuandika Programu za Kompyuta (Computer coding)
        - WoC’s
    - Wasichana Wanaoandika Programu (Girls Who Code)
    - Hisabati Inaongea (Math Speak )
- Ufafanuzi juu ya mafunzo – wenzako na wataalamu
- Kulinganisha (matching) – kufaa kwa kila kitu na utayari wa kubadilika kwa haraka
- Tathmini ya ujuzi – mgumu na mwepesi (hard & soft)| Usalama=
    - Ukaguzi wa nyuma, majukumu & mategemeo na mipaka
- Jambo lingine lolote linaloweza kuwa linahitajika kulingana na programu yako

**Hivi ni vidokezo**– Tazamahttps://www.youtube.com/user/mathantics
http://www.mentoringpittsburgh.org/pages/training-for-mentors
https://www.nationalacademies.org/our-work/the-science-of-effective-mentoring-in-stemm
https://codakid.com/coding-for-kids-the-ultimate-guide-for-parents-2/
Wazazi, mishtuko ya vizazi na watoto - https://www.sciencemag.org/news/2019/07/parents-emotional-trauma-may-change-their-children-s-biology-studies-mice-show-how| https://www.nctsn.org/

### XXXI. Jinsi ya kuwasaidia watoto kuwasilisha mawazo yao na kushinda zawadi?

Tazama sehemu C na kiungo kilichowekwa chini
https://ozobot.com/blog/26-tech-tools-teachers-can-use-inspire-classroom-creativity
https://www.rootsofaction.com/nurturing-childrens-creativity/

### XXXII. Jinsi ya kuandaa vijana na mikutano ya kimataifa

Fanya mazoezi ya kuwasilisha (pitching) kwa mwezi kabla ya mkutano wa kitaifa. Utajua mtoto yuko tayari, watakapoweza kupata watu zaidi ya 50 wanaoamini katika wazo lao.

Kufanya mazoezi ya mawazo mazuri, waambie watoto waandae mawazo mengi kadri wanavyoweza kwa kila siku kwa kuwauliza yafuatayo:

Kila siku, haijalishi una mtoto mmoja au la, fanya shughuli hii kukusaidia kufikiria kwa kina

- Tambua wazo moja kila siku na uliwasilishe mbele ya watu watano tofauti
  - Toa njia tatu ambazo unaweza kuzitumia kulikamilisha
- Yaweke kwenye boksi na kisha uyapitie tena kila Jumapili
  - Chagua wazo moja ambalo ni rahisi kutekelezwa na uliwasilishe mbele ya watu watano na kisha uwaulize kama wako tayari kutoa pesa au muda ili kulifanyia kazi – anza na watu wa karibu yako.
- Kila wiki boresha mawazo yako, huku ukiongeza kiwango cha pesa na muda ambacho unawaomba ili kukamilisha.
  - Tazama kiasi cha pesa ya zawadi katika mikutano ya WoC ili kukupa mwangaza.

**Jinsi ya kutambua mawazo bora ya kuwasilisha?**

1. Tambua wazo moja ambalo limepata watu 10-30 walio tayari kuwekeza ndani yake mfano limewasisimua au wako tayari kutoa pesa
   - Toa sababu tatu za namna utakavyo lifanya kuwa halisi na ufanye mazoezi
   - Ni nini kitakusaidia kulifanya kuwa halisi?
   - Ujuzi mmoja ambao unauhitaji ili kulifanya kuwa halisi
   - Ni ujuzi gani mmoja ambao unao, na una mpango gani wa kuutoa kwa mtu mwingine?

Kama wewe ni mzazi, mwalimu au kiongozi wa jamii, tuma wazo lako kwetu kupitia tovuti yetu na usubiri kuona kama wazo lako litachaguliwa kuwasilishwa kwa ajili ya kushinda zawadi. Fanya hivi kwa jamii yako KWANZA.

## XXXIII. Uhamasishaji wa Usalama Mtandaoni

Programu ya uhamasishaji wa ulinzi ya WoC inasaidia kutengeneza mazingira salama na ya ulinzi kwa kuhamasisha watoto juu ya hatari za kimtandao. Tunatoa nyenzo muhimu kama vile maarifa ya kupambana na adui na kufanya jamii nzima kuwa salama. Tazama sehemu ya 3 katika nyaraka hii kujua zaidi juu ya usalama. Programu inafundisha mada kama vile

- Phishing |Social Engineering | Faragha | Unyanyasaji wa mtandaoni | Tuma kwa akili timamu na zaidi |Adui habagui | Elimu endelevu |Mjadala |Ushiriki |Majadiliano ya darasani | Taarifa nyingi sana

Kila mtu anatakiwa kuweka kipaumbele kwenye usalama kila mahali




**Jifunze zaidi mtandaoni-**
**https://womenonchange.org/**

